OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KALAMBO
SHULE YA SEKONDARI MWIMBI

Baruapepe: *mwimbiss@gmail.com*
Mkuu wa Shule: 0757468056
blog: ***mwimbihighschool.blogspot.com***
Makamu Mkuu wa Shule
+255 757848072

S. L. P 100,
MATAI-KALAMBO
RUKWA

Tarehe: 29 **Machi**, 2022

KUMB.NA. KDC/MWSS/J1/FV/V011/2022/ 001

Jina la Mwanafunzi: ……
S.L.P. ……..
……..

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWIMBI KWA KIDATO CHA TANO MWAKA 2022/2023.**

l. Nafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha TANO katika Shule ya Sekondari Mwimbi , tahasusi ya**.....** (HGL na HGK) Tunakupongeza kwa mafanikio hayo.

Shule itafunguliwa tarehe …./…../2022, unatatakiwa kuwepo shuleni siku hiyo. Kutofika Shule kwa wakati uliopangwa kunaweza kukupotezea nafasi yako ya masomo.

Shule hii ipo katika Wilaya ya Kalambo, Mkoa wa Rukwa. Ipo kilomita 48 kutoka mji wa Matai ambao ni Makao Makuu ya Wilaya na Kilometa 99 kusini mwa mji wa Sumbawanga ambao ni Makao Makuu ya Mkoa wa Rukwa.

Kama unatokea njia ya Mpanda au Mbeya shuka stendi kuu ya mabasi Katumba- Sumbawanga, kisha panda mabasi yanayoelekea Ulumi (Mambwe) au Kalembe. Mabasi yanaondoka stendi kuu Katumba-Sumbawanga kati ya saa 6:00 na Saa 7:30 Mchana, nauli ni Tsh. 6,000/= waeleze unashuka Mwimbi. Ukishuka unaweza ukatembea kwa miguu kuja shuleni au chukua usafiri wa pikipiki kwa nauli ya Tsh. 1 ,000/= utaletwa mpaka shuleni.

Utapokelewa shuleni endapo utasoma vyema maelekezo na kukubaliana nayo na kutimiza mambo yaliyomo kwenye viambata vyote vilivyopo.

Tarehe ya mwisho ya kuripoti shuleni ni tarehe: …../…../2022

Ni matumaini yetu kwamba utasoma na kuzingatia maelekezo yote na mzazi/mlezi atakutimizia mahitaji yote kabla ya kuripoti shuleni ili kuepuka usumbufu usio wa lazima.

Pia tunategemea utafurahia maisha kwa muda wote utakaosoma hapa na kwamba utaonyesha tabia njema, utakuwa na ari ya kujifunza na utajitahidi kutekeleza shughuli zote zinazomhusu mwanafunzi kwa juhudi na maarifa. Walimu, wafanyakazi, wanafunzi wenzako na wanajumuiya wote kwa ujumla wapo tayari kukupa kila msaada utakaohitaji pale itakapolazimu.

2. **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

i. SARE YA SHULE

- **WASICHANA**
  a. Sketi mbili za kushonwa vizuri zenye urefu wa kufunika soksi fupi sentimeta tatu(3) kutoka kilipoishia kiatu, moja ya rangi ya kijivu na nyingine rangi ya brauni (ugoro).
  b. Mashati mawili (2) meupe (tomato) mikono mirefu
  c. Sweta moja (l) rangi ya zambarau lenye shingo (V).
  d. Viatu vyeusi jozi mbili (2) vya kufunga kwa Kamba/gidani visiwe na sori ndefu na visivyochongoka mbele.
  e. Soksi jozi mbili nyeupe
  f. Raba nyeupe kwa ajili ya michezo
  g. Tracksuit rangi ya darkblue (Adidas) isiyobana kwa ajili ya maandalizi ya jioni.
  h. Necktie mbili zenye rangi sawa na za sketi.
  i. T-shirt ya shule (zinapatikana shuleni kwa tshs 12,000/- kila moja)
  j. Hijabu tetron nyeupe/juba na siyo mtandio isiwe na urembo wowote. Pia isiwe na urembo wa lessi (**kwa Wanafunzi wa Kiislamu tu**)
  k. Gauni la kazi lefu (Shamba Dress) rangi ya zambarau mshono wa solo **LISILOBANA** . Ziwe mbili (2). ***Tazama picha na mchoro ukurasa wa mwisho, tunashauri tumia wino wa rangi ili upate rangi halisi ya mavazi***

ii. ADA NA MICHANGO YA SHULE

a. Ada ya shule ni tshs. 70,000/- (sabini elfu tu) kwa mwaka. Anaweza kulipa (tshs 35,000/-) kwa muhula na inayobaki akalipa muhula wa pili. Ada ilipwe kwenye akaunti ya shule namba **62101100104, (Mwimbi Secondary School Revenue collection-NMB**). Hatupokei fedha mkononi. Uje na bank-pay-in-slip, Tafadhari andika jina la Mwanafunzi kwenye bank pay-in-slip.
b. Tshs. 20,000/- kwa ajili ya mitihani ya kujipima (Mock Examinations).

iii. MICHANGO MINGINE UNAYOPASWA KULIPA

(*Michango hii ilipwe kupitia Akaunti Namba* ***62110030474 (Mwimbi Secondary Self Reliance- NMB)***

i. Tshs. 15,000/- kwa ajili ya ukarabati wa samani kwa mwaka.

ii. Tshs. 6,000/- kwa ajili ya kitambulisho na picha.

iii. iii. Tshs. 20,000/- mchango wa taaluma kila mwaka.

iv. Tsh. 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine (kila mwaka)

v. Tsh. 10,000/-kwa ajili ya huduma ya kwanza (5,000), na CHF Tsh.5000/- (Kila mwaka).

vi. Tsh. 5,000/- ya Tahadhari (haitarejeshwa).

iv. Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni

- **MAHITAJI YA DARASANI**

a) Ream ya karatasi (A4) moja kwa mwaka (aje nayo).
b) Vitabu vya masomo ya History, General Studies, Kiswahili, Geography, na English Language kutegemeana na tahasusi uliyochaguliwa.
c) Nakala ya result slip.

d) Koti la mvua/ mwavuli
e) Madaftari 10 (counter Books)
f) Graph pad moja kwa watakao soma Geography
g) Kalamu/Penseli za kutosha
h) Mkebe wa hisabati (Mathematical Set)- kwa watakaosoma Geography
i) Begi imara la kubebea daftari

- **MAHITAJI WA BWENINI**

a) Godoro moja ft 2 1/2 x 6.
b) Shuka 2 rangi ya pink
c) Mto na foronya 2 za pinki
d) Blanket moja (students size.)
e) Chandarua kwa ajili ya kujikinga na mbu
f) Taulo, soksi na koti (**nyeusi)** zito kwa ajili ya baridi
g) Pull-neck Nyeusi kwa ajiri ya baridi (dharula za kiafya kwa wenye mahitaji maalumu ya kiafya)
h) Ndoo mbili za lita 10
i) Sanduku imara la bati moja lenye makufuli mawili
j) Vyombo vya chakula (Container la chakula, Kijiko, kwa wale wenye changamoto Zaidi za kiafya wanaweza kuja na Chupa ya Chai ndogo kwa ajili ya dharula za kiafya.
k) Kandambili kwa ajili ya kuogea
l) Viatu vya wazi vyeusi vya plastiki (Cat sandals) kwa ajili ya kushindia
m) Vifaa vya usafi (kwanja, jembe lenye mpini, reki, drier, fagio ya ndani na wa nje, brush ngumu ya usafi wa chooni)

NB: Masanduku/Mabegi Makubwa ya nguo **HAYARUHUSIWI,** kwani hatuna nafasi ya kuyatunza. Mwanafunzi asije na mavazi mengine zaidi ya hayo yaliyoelekezwa (yaani aje na Uniform, Shamba Dress, Track-Suit, T-shirt Na Khanga/Kitenge Doti Moja Tu kwa Wasichana) akija nalo atalazimika kurudishwa nyumbani kwa gharama zake.

3. **SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE**

Sheria na kanuni hizi zinazingatia misingi ya HESHIMA, ADABU, UAMINIFU, UTII na TABIA NJEMA kwa ujumla.

Wanafunzi wanatazamiwa kuwa mfano mzuri kwa heshima, tabia, kauli na vitendo. Hivyo:-

1. Mwanafunzi atasimama anapomsalimu Mwalimu, Mtumishi wa shule au mtu yeyote aliyemzidi umri.
2. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi kutumia lugha chafu au ya kihuni popote na wakati wowote hata kwa wanafunzi wenzake.
3. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi
    a) Kufuga kucha au nywele
    b) Kufuga ndevu
    c) Kunyoa kipara
    d) Kutukana
    e) Kutia dawa nywele (curly) na kujichubua ngozi ya mwili kwa madawa
    f) Kuvaa vitu kama mapambo mfano Heleni, Mikufu bangili au vitu vya kiimani kama Vile Rozali, Kofia, Kanzu, Vilemba, Suruali fupi kwa kuwa Shule hii ni ya Serikali.

g) Kuvaa viatu vya soli nene na ndefu
h) Kuvaa kaptura na kandambili kwenye Bwalo la chakula na Ofisi zote za shule i) Kuvaa sketi fupi
j) Kuvaa suruali chini ya kiuno
k) Kuvaa nguo za mtindo, mfano:- suruali za kubana/chupa/jeans/

4. Mwanafunzi atasimama kwenye mstari wakati wa kupata huduma
5. Mwanafunzi atanyoosha mkono juu na kusimama anapouliza au kujibu swali
6. Anatakiwa kuwa mtulivu asipige kelele au vitendo vyovyote vitakavyo sababisha usumbufu kwa wengine anapokuwa Darasani Maktaba, bwenini, wakati wa kujisomea (prep) na katika mikusanyiko yoyote.
7. Mwanafunzi LAZIMA awahi na ahudhurie mahali anapotakiwa katika shughuli za shule.Hivyo Mwanafunzi:-

    A. Aripoti shuleni tarehe ya kufungua shule na kujiandikisha rasmi siku na saa ya kuripoti kwa mwalimu anayehusika.
    B. Ahudhurie vipindi vyote darasani kama ilivyopangwa
    C. Ahudhurie kwenye kazi atakazopangiwa
    D. Ahudhurie kwenye paredi ya uhakiki wa uwepo wake shuleni (Roll call). Ukaguzi wa Usafi , kupandisha Bendera ya Taifa, Mikutano ya nyumba, Mikutano ya darasa na Maabara za shule.

8. NI LAZIMA mwanafunzi awe katika sare ya shule na awe na KITAMBULISHO kwa nyakati zote awapo shuleni na nje ya shule kama:- Anapotoka nje ya shule kwa ruhusa maalumu kwenda kanisani, msikitini,hospitali, likizo au kwa shughuli yoyote itakayomlamzimu kwenda nje ya shule.
9. NI LAZIMA mwanafunzi awe ndani ya mipaka ya shule wakati wote isipokuwa akiruhusiwa kuwa nje ya mipaka ya shule kwa ruhusa maalumu, na atapaswa kuwa na kibali (pass) cha maandishi.
10. Mwanafunzi lazima ahudhurie prep inayoanza saa 1:300 jioni na awe kitandani kwake wakati wa kuzima taa (lights out) saa 4:30 usiku.
11. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia umeme kwa shughuli yoyote ile awapo bwenini au darasani.
12. Hairuhusiwi kufanya mikutano yoyote shuleni pasipo kibali cha Mkuu wa Shule na ikiwa kibali kimetolewa kikundi au chama kitatakiwa kuandika muhtasari wa kikao na nakala kuwasilishwa kwa Mkuu wa Shule.
13. USAFI: Mwanafunzi anawajibika kuwa msafi lava mavazi na mwili wake na kushiriki kuyaweka mazingira ya shule katika hali ya usafi.
14. Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare za Shule ya Sekondari Mwimbi muda wote akiwa ndani na nje ya shule na achomekee shati lake. Mavazi yasiyo ya shule hayaruhusiwi kabisa.
15. Hairuhusiwi kujihusisha na mikutano ya siasa katika kipindi chote awapo rnwanafunzi.
16. MAENEO YASIYORUHUSIWA: Mwanafunzi haruhusiwi kufika/ kuingia sehemu zifuatazo bila ruhusa maalumu:
    a) Ofisi za shule
    b) Bohari za shule
    c) Kwenye disco, ngoma , muziki au kwenye sherehe yoyote ndani na nje ya shule d) Maabara.
    e) Baa,kilabuni au mahali popote panapouzwa pombe au vileo vingine
    f) Nyumba za wageni (Guest House)
    g) Nyumba za watumishi/walimu

ZINGATIA:

Unataarifiwa kuwa shule hii ni shule ya Serikali. Aidha inazingatia Katiba ya nchi kuhusu uhuru wa kuabudu, hivyo wanafunzi huruhusiwa kwenda sehemu za ibada kulingana na imani zao. Pia kumepangwa vipindi viwili vya dini katika ratiba ya masomo kwa siku ya ijumaa na kila siku jioni baada ya chakula kuanzia saa 1:00 hadi saa 1:30 jioni. Wanafunzi hawaruhusiwi kuanzisha ratiba yao

ya kuabudu katikati ya vipindi na ratiba zingine za shule. Tofauti ya hayo Mzazi/Mlezi anashauriwa kumtafutia mwanafunzi shule ya seminari endapo mwanafunzi huyo ana wito wa dini husika.

MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE:

1 . Wizi
2. Uasherati, ushoga na ulawiti,ubakaji
3. Ulevi wa aina yoyote kama utumiaji wa madawa ya kulevya, pombe, sigara,bangi, mirungi n.k 4. Makosa ya jinai
5. Kuoa au kuolewa
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7. Kupigana au kumpiga mwingine.
8. Kudharau Bendera ya Taifa
9. Kulala nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa shule
10. Kuchochea, kuandamana, kufanya vurugu au kugoma kwa namna yoyote
11. Kutoa lugha ya matusi
12. Kumdharau kiongozi wa shule, Mwalimu, Mfanyakazi na jamii kwa ujumla
13. Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki pasi ya umeme, heater, simu au sehemu ya simu kama laini, Charger, memorycard, flash nk
14. Kukosa kuhudhuria vipindi darasani na au kutofanya mitihani na majaribio kwa makusudi.

NB: **kwa mwanafunzi anayetoka mbali ataruhusiwa kuja na simu kwa ajili ya mawasiliano na mzazi wake akiwa safarini kwa muhula wa kwanza tu, baada ya hapo HATARUHUSIWA kuja na simu kwa vyovyote vile**.

KARIBU SANA MWIMBI SEKONDARI.

……

MWL. ESTHER E. MALLYA

MKUU WA SHULE.

THE HEADMASTER MWIMBI SECONDARY SCHOOL P.O. BOX 100 KALAMBO

PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KALAMBO DISTRICT COUNCIL
MWIMBI HIGH & SECONDARY SCHOOL,

P.O. Box 100,
Kalambo-Rukwa.

Date :..../...../2022.

MEDICAL EXAMINATION FORM

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FOR A FORM V STUDENT Please examine the named below as to his/her fitness for admission to school as a form V student.

To be completed by a Government Medical Officer in respect of FORM V entrants:

Pupil's Full Name.... . . . . .……
.Blood count (Red and White). . . . . ……
Stool Examination…… .
Urinalysis.... . . . . ……
Syphilis Test ……..
T. B. Test……
Eye Test……
Ears.... . . . ……..
Chest.... . . . . ….. . . . . .
Spleen. . . . . ..……
Abdomen. . . . . ……
Blood Group.... . . . . ……
Pregnancy..... .....
ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical defects or impairments infections, chronic or family diseases etc.

_____

_____

I have examined the above named and I consider that he/she is physically fit/unfit to pursue as stated above.
Name and signature of Certifying Officer.

Name …… Signature.... . . . . ……... . . . ……

.Station ……..…….....Designation ……. . . . . ……

Date . . . . . ……. STAMP……

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI MWIMBI

FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI PAMOJA NA AHADI YA UTII WA SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

1. Jina kamili kama lilivyo kwenye selform.....
2. Anuani ya nyumbani S. L. P..... Wilaya ya.....Mkoa wa……
3. Tarehe ya kuzaliwa.....Mahali ulipozaliwa.....Kijiji/Mtaa……
4. Mahali unapoishi sasa.....Wilaya ya..... Mkoa wa..... .
5. Shule ya sekondari ulikotoka na anuani yake……..
6. Dini/ dhehebu..... Kabila ……..
7. Jamaa katika familia ambao wanaweza kupelekewa taarifa zako ,uhimu kwa masuala yahusuyo shule:
   i. Jina la Baba……. Namba ya simu:.....

Hai/Si hai.....(kama hai) kazi yake.....Anuani yake:..... ii. Jina la mama:..... Namba ya simu…….. Hai/si hai..... (kama hai) kazi yake.....Anuani yake..... ..... iii. Jina la Mlezi..... Namba ya simu.....,,..... Hai/Si hai.....(kama hai)kazi yake.....Anuani yake…….

NB: BANDIKA PICHA ZA PASSPORT SIZE KWENYEVIBOMA VYA WATAJWA HAPO JUU

PICHA YA BABA	PICHA YA MAMA	PICHAYA MLEZI

Mimi (mwanafunzi).....nathibitisha kuwa taarifa nilizotoa hapo juu ni za kweli. Ahadi yangu, nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa ya kujiunga na shule hii ili baadaye niweze kulitumikia Taifa langu, hivyo naahidi kufuata sheria na kanuni za shule kama zzilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi na shule.

……. ……/…../2022
Saini ya Mwanafunzi Tarehe

Mimi(Mzazi/mlezi wa mwanafunzi) …….....ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi, nimezisoma sheria na kanuni za shule ya sekondari Mwimbi ambako kijana wangu amechanguliwa kujiunga na kidato cha Tano. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Naahidi kwamba nitamhimiza mwanangu kufuata sheria na kanuni zote za shule kama zilivyoelekezwa. Pia naahidi kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi bora ya mwanangu ili baadaye awe bora na mwema kwa Taifa.

…….. ……./…/2022
Saini ya mzazi/mlezi Tarehe

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KALAMBO
SHULE YA SEKONDARI MWIMBI.

Baruapepe: mwimbiss@gmail.com
Mkuu wa Shule:
+255 759 944 210, +255 676 208 124

Makamu Mkuu wa Shule
+255 755 569 494

S. L. P 100,
MATAI-KALAMBO
RUKWA

Tarehe: 29 Machi 2022

AINISHO LA ADA NA MICHANGO KWA KIDATO CHA TANO

No.	Aina ya Malipo	Muhuıa	Muhula 11	Jumla	Nimelİpa	baki
I	Ada a Shule kila mwaka	35,000/-	35,000/-	70,000/-		
2	Taaluma	20,000/-		20,000/-		
3	Ukarabati wa Samani	15,000/-		15,000/-		
4	Watumishi na vibarua wengine	30,000/-		30,000/-		
5	Matibabu	10,000/-		10,000/-		
6	T-shirt yenye Nembo	12,000/-		12,000/-		
7	Kitabulisho na picha	6,000/-		6,000/-		
8	Mtihani wa mock (akiwa kidato cha sita	20,000/-		20,000/-		
9	Tahadhari (hairudishwi)	5,000/-		5,000/-		
			Jumla	**188,000/-**		

.....
ESTHER E. MALLYA
Mkuu wa Shule.

THE HEADMASTER
MWIMBI SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 100
KALAMBO

SHULE YA SEKONDARI MWIMBI
MCHORO NA MFANO WA SALE YA SHULE

1. SKETI ZA DARASANI (ZIWE MBILI)

- marinda mbele na nyuma
- marinda madogo mawili pande zote mbili
- rinda boksi au rinda pana kubwa moja mbele na nyuma





GAUNI LA KAZI/KUSHINDIA (SHAMBA DRESS) ZIWE MBILI
- Gauni la kazi (Shamba Dress) iwe mshono wa solo
- Rangi Zambarau isiyobana (kifua/mwili kwa ujumla)
-Urefu toka kwenye kisigino hadi kwenye pindo la gauni usizidi sentimeta 18

Uniform 1 Shamba dress Uniform-2